VI. Maji ya jumla (Bulk Purchase) kutoka kwa wazailishaji wakubwa mfano (KASHWASA).

Gharama za uendeshaji na matengenezo zimetofautiana kutokana na mfumo wa uzalishaji wa maji.

### Bei zilizoidhinishwa na Bodi ya RUWASA

RUWASA kupitia kikao chake cha bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika tarehe 25/06/2021 Iliidhinisha bei za ukomo kwa vyombo vyote vya watoa huduma ya maji Vijijini kwa kuzingatia teknolojia mbalimbali zinazotumika katika miradi ya Maji vijijini baada ya kufanya tathmini ya kina ya bei zinazotozwa na vyombo vya watoa huduma ngazi ya jamii kwa sasa.

**JEDWALI 'A': BEI KIKOMO ZITAKAZOTUMIWA NA VYOMBO KWA WATEJA WENYE DIRA ZA MAJI**

| MFUMO/NISHATI INAYOTUMIKA KUSUKUMA MAJI | BEI ZA UKOMO KWA MITA MOJA YA UJAZO (SH) | BEI ZA UKOMO KWA NDOO YA LITA 20(SH) |
|---|---|---|
| MAFUTA | 2,500 | 50 |
| UMEME JUA | 1,500 | 30 |
| MSEREREKO | 1,000 | 20 |
| UMEME WA TANESCO | 2,000 | 40 |
| PAMPU YA MKONO | 1,000 | 20 |
| UNUNUZI WA MAJI YA JUMLA (BULK PURCHASE) | 2,500 | 50 |

**JEDWALI 'B': BEI ZA MAJI ZA UKOMO ZITAKAZOTUMIWA NA VYOMBO VYA WATOA HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII VISIVYO NA DIRA ZA MAJI**

| MFUMO/NISHATI INAYOTUMIKA KUSUKUMA MAJI | BEI ZA UKOMO, "FLAT RATE" KAYA KWA MWEZI (SHILINGI) |
|---|---|
| MAFUTA | 15,000 |
| UMEME JUA | 7,000 |
| MSEREREKO | 5,000 |
| UMEME WA TANESCO | 10,000 |
| PAMPU YA MKONO | 5,000 |
| UNUNUZI WA MAJI YA JUMLA (BULK PURCHASE) | 15,000 |

Aidha bei hizo zitaendana na masharti yafuatayo

(a) Chombo chochote hakitaruhusiwa kutoza bei zaidi ya zilizoainishwa katika Jedwali **"A" na "B".**

(b) Chombo chochote ambacho kinatoza bei chini ya bei kikomo kitaendelea kutoza bei ya awali na hakiruhusiwi kuongeza bei pasipo kupata idhini ya RUWASA.

(c) Chombo kinachotumia teknolojia zaidi ya moja katika uzalishaji wa maji kitatakiwa kutumia bei kikomo ya teknolojia inayochukua asilimia kubwa katika uzalishaji.

(d) Kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Vyombo vyote vinatakiwa kuwa vimefunga dira za maji kwa wateja wake wote.

(e) Kwa wateja wa majumbani na taasisi bei zitakuwa asilimia 70 ya bei kwa kila teknolojia kama zilivyoainishwa katika jedwali **"A" na "B"**

(f) Bei kwa wateja wa biashara na viwanda zitabaki kama zilivyoainishwa katika majedwali **"A" na "B"**

(g) Vyombo ambavyo vitashindwa kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi vinayoisimamia kutokana na bei kikomo zilizoainishwa katika Jedwali **"A" na "B"**, viwasilishe maombi ya bei maalum kwa kufuata utaratibu uliotolewa kwenye Mwongozo wa Upangaji wa Bei wa mwaka 2020 *(Tariff Setting Guidelines, 2020).*


Benki ya NBC, Tawi la Mazengo,
Barabara ya Kuu,
S.L.P 412, 40473 DODOMA
*Simu*: +255 (26) 23232563 / 4
*Barua Pepe:* dg@ruwasa.go.tz


**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAJI**

RUWASA

**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI RUWASA**

# UCHAMBUZI WA BEI ZA MAJI KWENYE VYOMBO VYA WATOA HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII



## Utangulizi

RUWASA ilianzishwa kwa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na 5 ya mwaka 2019 “The Water Supply and Sanitation Act, (No.5 of 2019)” ikiwa na lengo la kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira kwa wananchi waishio Vijijini.

Katika ngazi ya jamii huduma ya maji inatolewa kupitia vyombo mbalimbali (Consumer Association-CBWSOs, Trustees, NGOs, Cooperative Society, Campany). Vyombo hivi vipo katika maeneo mbalimbali yanayosimamiwa na RUWASA mikoani na wilayani Tanzania Bara. Katika kutekeleza jukumu hili vyombo hivyo vina jukumu la kasimamia miradi mbalimbali yenye vyanzo tofauti vya uzalishaji wa maji na kuhakikisha majisafi yanawafikia wananchi kwenye maeneo yao. Vyombo hivi vinatoa huduma kwa kujiendesha kutokana na mapato yatokanayo na mauzo ya maji.

Kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na 5 ya mwaka 2019, utaratibu umeruhusu kila chombo kupanga bei za maji ambazo zitakidhi gharama za uendeshaji, matengenezo na upanuzi wa miradi ya maji kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi na kipato cha wananchi.

Hapo awali mfumo uliokuwa unatumika kabla ya Sheria ya Huduma za Maji na usafi wa mazingira na 5 ya mwaka 2019 vyombo vinavyosimamia huduma ya maji vilikuwa vinapanga bei kwa kushirikiana na Mhandisi wa maji wa Halmashauri ya Wilaya/Manispaa ambapo Mhandisi alikuwa na jukumu la kukokotoa bei kwa kuzingatia gharama za uendeshaji na matengenezo ya skimu ya maji na bei hizo kuwasilishwa katika Mkutano Mkuu wa watumia maji wa Kijiji husika na mwenyekiti wa chombo cha watumia maji kwa ajili ya kupewa idhini ya matumizi.

Kwa sasa kupitia sheria ya Huduma za Maji na usafi wa Mazingira na 5 ya mwaka 2019, Kanuni ya 26 inaipa Bodi ya RUWASA mamlaka ya kuidhinisha na kudhibiti bei za vyombo vya watoa huduma ya Maji Ngazi ya jamii kwa kuzingatia mwongozo wa kupanga bei (Tariff setting guidelines 2019).



## Ukokotoaji wa bei za Maji Vijijini

Kwa mujibu wa muongozo wa upangaji bei, Mambo yafuatayo huzingatiwa wakati wa uchambuzi na tathmini: -

(i) Gharama za uendeshaji na matengenezo;
Gharama hizi zilitumika kama zilivyowasilishwa katika na vyombo vya watoa huduma ngazi ya jamii ambapo gharama hizi ziliwasilishwa kama wastani kwa mwezi.

(ii) Gharama za uchakavu;
Gharama za uchakavu zilikokotolewa kwa kutumia asilimia 80 ya gharama ya mradi na kugawanywa kwa muda sanifu wa mradi (Design period) ambayo ni sawa na asimia 4 tu za gharama ya mradi ndiyo zilikadiriwa kuwa gharama za uchakavu (Kwa dhana ya kuwa uchakavu ni vifaa vya Electro Mechanical pekee) aidha muda wa mradi timu ilichukua miaka 20 kama inavyoelekezwa katika mwongozo wa usanifu wa miradi

(iii) Mahitaji ya upanuzi wa mradi na matengenezo makubwa; Mahitaji ya upanuzi yalichukuliwa kwa kuzingatia asilimia kumi ya gharama za mradi ukijumuisha na gharama za uchakavu na kugawanywa kwa 20 kama muda wa usanifu wa mradi,

(iv) Gharama za matumizi mengineyo/dharula.
Gharama hizi zilipatikana kwa kuchukua asilimia 5 ya mahitaji yote ya gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi kwa mwaka.

(v) Upotevu wa Maji
Hii inapatikana kwa kuchukua asilimia 20 ya maji kwa vyombo vyote kama inavyoelekezwa katika muongozo wa upangaji wa bei.

Aidha uchambuzi wa bei hulenga katika kupata makisio ya tozo zitakazowezesha upatikanaji wa huduma endelevu ya maji katika jamii.

## Maelezo ya kina ya uchambuzi na ukokotoaji wa bei

Uchambuzi na ukokotoaji wa bei huzingatia kila teknolojia ya uzalishaji wa maji ambapo kila teknolojia imechanganuliwa kipekee kutokana na utofauti wake katika mahitaji ya fedha kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo.
Teknolojia zinazotumika katika miradi ya maji vijijini ni:-

I. Mserereko

II. Kusukuma maji kwa kutumia nishati ya umeme wa Grid ya Taifa

III. Kusukuma maji kwa kutumia nishati ya umeme jua

IV. Kusukuma maji kwa kutumia nishati ya mafuta

V. Pampu ya mkono